BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Pili – Tarehe 07 Mei, 2026
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2026/2027.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa Mwaka 2026/2027.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

335. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Tafiti za kitaaluma na zisizo za kitaaluma ni nyenzo muhimu katika kusaidia Serikali kufanya maamuzi sahihi ya kisera na maendeleo. Kwa mujibu wa taratibu zilizopo, watafiti hupewa vibali vya kufanya

tafiti zao Zanzibar na hutakiwa kuwasilisha nakala za tafiti zao baada ya kukamilika.

(a) Ni tafiti ngapi zimetolewa vibali na kufanywa Zanzibar katika kipindi cha miaka mitano (2020-2025).

(b) Je, matokeo na mapendekezo ya tafiti hizo yanatumika vipi katika kuboresha sera, mipango na maamuzi ya Serikali.

(c) Je, kuna utaratibu gani wa kufuatilia uwasilishaji wa nakala za tafiti, hususani zile zinazofanywa na wageni.

## Ofisi ya Rais - Ikulu:

193. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu:

Kazi ni kipimo cha utu na kila Mzanzibari ndani ya nchi hii anapambana kupata haki yake ya kufanya kazi, iwe kwenye taasisi binafsi au Serikalini, ili kujipatia kipato cha halali na kuzidi kuinua uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo, kunaongezeka malalamiko mengi kwa sasa, pale linapokuja suala la uhakiki (Vetting) kutoka katika Ofisi ya Usalama wa Serikali (GSO), hali inayopelekea vijana wengi kukosa nafasi za kuitwa kazini kwa vigezo ambavyo sio vya msingi.

(a) Je, Serikali mpaka sasa imepokea malalamiko mangapi juu ya kadhia hii na imechukua hatua gani kulitafutia suluhisho suala hilo.

(b) Ni kwa kiasi gani GSO hutekeleza wajibu wake bila ya upendeleo.

(c) Ni ipi ahadi ya Serikali kwa vijana wote wa Zanzibar juu ya kunufaika na fursa za ajira Serikalini bila ya upendeleo wa kisiasa.

## Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

454. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ:

Licha ya uwepo wa Wabunge, Wawakilishi na Madiwani katika majimbo yetu, wapo Masheha ambao wanafanya kazi kubwa sana katika kuzisimamia jamiii zetu na kuwa kiunganishi baina ya Serikali na jamii, kama ilivyo pia baina ya wanasiasa na jamii.

(a) Ni upi mpango wa Serikali wa kuboresha maslahi ya Masheha yatakayoendana na ugumu wa kazi zao.

(b) Ni lini Serikali itawapatia Masheha usafiri utakaowasaidia katika ufuatiliaji wa kazi zao za kila siku.

**Wizara ya Fedha na Mipango:**

349. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipago:

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) ni miongoni mwa Mifuko muhimu sana ya kuwahudumia wananchi baada ya kustaafu, ambapo pamoja na mambo mengine, miongoni mwa faida wanazotakiwa kupata wachangiaji wa Mfuko huo ni fao la matibabu.

Je, ni wananchi wangapi wamefaidika na fao la matibabu kupitia Mfuko wa ZSSF.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

39. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Mnamo tarehe 19 Novemba, 2025 Wizara ya Maji, Nishati na Maadini iliwaandikia barua Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wenye majimbo, kuainisha changamoto za maji katika majimbo yao. Tangu kutolewa kwa barua hiyo, changamoto ya uhaba na ukosefu wa maji imezidi katika majimbo mbalimbali.

Je, hatua za utatuzi wa changamoto hizo zimekwama wapi.

123. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Hivi karibuni Serikali kupita Wizara ilitoa taarifa ya kuweka viwango vya faini kwa gari zitakazokiuka utaratibu wa kupakia mchanga. Hatua hiyo, imeleta maswali kwa wadau wa nishati hiyo kama imezingatia utaratibu sahihi wa kisheria.

(a) Je, ni kanuni gani zimeweka viwango vya faini vilivyotangazwa na Wizara.

(b) Je, kanuni hizo zimepitiwa na Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Kanuni na Sheria Ndogo.

(c) Na kama kanuni hizo hazipo au hazijapitiwa na Kamati husika ya Baraza, ni upi uhalali wa tangazo la Wizara.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

372. MHESHIMIWA MAKAME MOHAMED SUFIANI (Jimbo la Chumbuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kuna ongezeko kubwa la wageni hapa nchini kwetu ambao wanaitumia ardhi yetu kwa kuishi pamoja na familia zao, bila ya Mikataba ya Ukodishaji.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwatambuwa wageni hao.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kukusanya mapato hayo.

**Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

4. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Kwa muda mrefu sasa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) halitowi mgao wa fedha kwa Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), mgao unaotoka Shirikisho la Soka Ulimwenguni (FIFA), Shirikisho la Mpira wa Miguu Barani Afrika (CAF) ama misaada wanayoipata nje ya nchi kwa madai kuwa, michezo sio suala la Muungano na ZFF sio mwanachama halali wa taasisi hizo duniani.

(a) Kwa kuwa fedha hizo huja kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni lini Serikali itaingilia kati kuisaidia ZFF kuzidai pesa hizo kutoka TFF.

(b) Je, Serikali ina uhakika upi wa ZFF kupata mgao wake kutoka TFF iwapo itajiunga na kuwa mwanachama halali wa FIFA na CAF.

(c) Ni upi msimamo na kauli ya Serikali juu ya ZFF kutopata gawio lolote kutoka TFF, FIFA wala CAF.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

345. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Hivi karibuni tumeshuhudia kushamiri kwa matokeo mengi yanayokosa misingi ya utu na maadili ya utamaduni wa Zanzibar katika skuli binafsi, kama vipigo visivyozingatia miongozo ya Wizara na wakati mwengine husababisha madhara makubwa na hata vifo, ukamatishwaji wa mbwa kwa wanafunzi na mambo mengine.

Kwa kuwa Serikali inavifahamu vitendo hivyo, imechukua hatua gani kukomesha vitendo hivyo.

387. MHESHIMIWA DKT. NASRA NASSOR OMAR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kuna malalamiko kuwa baadhi ya walimu hawapati posho ya likizo kwa muda mrefu sasa.

(a) Je, Serikali inahakikisha vipi kuwa walimu wote wanapata posho ya likizo kwa wakati na kwa usawa.

(b) Ni hatua gani huchukuliwa kwa mwalimu ambaye hajapata posho hiyo kwa muda mrefu.

**Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:**

12. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Katika nchi yoyote, maendeleo endelevu hujengwa kwa kuwashirikisha wananchi katika shughuli za uzalishaji mali na kuinua hali zao za maisha.

Je, ni kwa kiasi gani wananchi wanashirikishwa katika shughuli za uzalishaji mali.

**<u>Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:</u>**

311. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Serikali ilianzisha Mfumo wa Anuani ya Makaazi ambao unatarajiwa kuwa nyenzo muhimu katika kuboresha utambuzi wa makaazi, kurahisisha utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi, pamoja na kuimarisha mifumo ya kisasa ya biashara na utawala.

(a) Je, utekelezaji wa Mfumo wa Uwekaji wa Namba za Nyumba umefikia hatua gani kwa Unguja na Pemba hadi sasa.

(b) Serikali inatarajia kukamilisha lini mfumo huu, ili uanze kutumika kikamilifu katika utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi kwa wananchi.

(c) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuunganisha mfumo wa Anuani za Makaazi na mifumo ya Kidijitali ya Serikali.

**<u>Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:</u>**

100. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kwa kuwa hali ya usalama katika dunia imekuwa inabadilika kila wakati na matukio ya uhalifu wa kimataifa yanachukuwa sura mpya ya kutumia udhaifu wa uingiaji na utokaji katika nchi mbalimbali. Na kwa kuwa Zanzibar ina bandari bubu nyingi ambazo watu kutoka nje ya visiwa vya Zanzibar, wakiingia kwa vyombo vya kienyeji bila ya ukaguzi wa kutosha. Na kwa kuwa kutokudhibitiwa kwa hali hiyo, kutatoa fursa itakayotumiwa na wahalifu wa kimataifa kupenya na kufanya matendo ya kihalifu.

(a) Serikali imeshafanya tafiti zipi za kujuwa idadi ya bandari bubu zilizopo Zanzibar.

(b) Kwa kuwa hivi sasa Madiko ya Uvuvi pia yanatumika kusafirisha watu kwa vyombo vya uvuvi, kuna hatua gani za udhibiti zimeanzishwa, ili kukinga madhara ya uingiaji wa watu kiholela.

(c) Kwa Serikali kuchelewa kuchukuwa hatua katika jambo hili, je, haioni kuwa inafuga tatizo ambalo baadae litakuwa kubwa kudhibiti madhara yake.

249. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

(a) Serikali ina mpango gani wa kununua *pilot* pamoja na *tag boats,* kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma na kuongeza ufanisi katika bandari za Zanzibar.

(b) Ni lini Serikali itapeleka wataalamu wa kuingiza na kutoa meli (pilots), katika bandari ya Mkoani ambayo inakabiliwa na changamoto hiyo pamoja na vitendea kazi muhimu.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

492. MHESHIMIWA MOZA MOHAMED KHAMIS (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Hospitali ya Abdalla Mzee inakabiliwa na changamoto ya jenerata, ambapo jenerata liliopo sasa ni la *manual* na umeme wetu hauna dhamana, hivyo hupelekea matatizo mbalimbali kwa wagonjwa.

Ni lini Serikali itatembelea hospitali hiyo na kubadilisha jenereta hilo kuwa *automatic*, ili umeme ukizimwa liweze kuwaka na kuendelea na huduma.

**<u>Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>**

289. MHESHIMIWA ALLEY MASOUD ALLEY (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Kwa kuwa suala la uwepo wa mafuta na gesi asilia limekuwa likizungumzwa kwa muda mrefu hapa Zanzibar, wananchi wanataka kufahamu ukweli wake.

(a) Je, rasilimali hizo zipo au hazipo.

(b) Kama zipo, ni lini wananchi wa Zanzibar wanatarajia kuanza kunufaika nazo.

(c) Na kama hazipo, ni lini Serikali itatoa taarifa rasmi ili kuondoa sintofahamu iliyopo kwa wananchi.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2026/2027.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2026/2027.

Zanzibar,
07 Mei, 2026.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA LA
WAWAKILISHI, ZANZIBAR